HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI NKUYU,

S. L. P 02,

KYELA

KUMB NA. NKY/S.2294/J. 1/2020

MWANAFUNZI: ……..

……

S. L. P …….

……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NKUYU WILAYA YA KYELA, MKOA WA MBEYA MWAKA 2020.

1.0.UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na **KIDATO CHA KWANZA** katika Shule hii mwaka 2020. Shule ya Sekondari Nkuyu ipo umbali wa Km 2 ½ Kaskazini mwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 06/01/2020, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 07/01/2020 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2020.

2.0.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. SARE ZA SHULE.

(a) Sare ya shule ni suruali ya Kaki moja na Suruali Damu ya Mzee moja kwa Wavulana na Sketi moja ya Kaki na Sketi moja ya Damu ya Mzee kwa wasichana.

- Maelezo ya mshono : Rinda box kubwa 2 ndogo 8 iguse kiatu kwa wasichana. Shati nyeupe mikono mifupi kwa Wavulana na wasichana

(b) Rangi ya Hijabu ifanane na rangi ya shati (Nyeupe)

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni T – Shirt bluu moja na Bukta bluu moja kwa Wavulana na T – Shirt bluu moja na bukta bluu moja kwa Wasichana.

2.2. Daftari kuanzia quire 2, kalamu na mkebe wa hesabu

3.0. Sheria na Kanuni Muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi a utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
i) Kutunza mali za umma

3.2. Makosa Yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0. Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

5.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekelezza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……..

MKUU WA SHULE

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI NKUYU S. L. P 2, KYELA

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina Kamili ……..……....
2. Tarehe ya kuzaliwa ……..……
   (tarehe, mwezi na mwaka)
3. Kabila ……..…….....
4. Taifa …….....
5. Dini …….....
6. Jina kamili la Baba ……
7. Anuani ya Baba ……
8. Jina kamili la Mama ……
9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana? ……
10. Kazi ya Baba: ……
    (i) Jina na anuani ya mlezi wako (kama sio/mzazi)

    ……..

    (ii) Namba ya simu ya mzazi …….....
    (iii)Kama ni mlezi uhusiano wako naye ukoje? …….

    …….....

11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi? (Taja sehemu moja tu utakapokwenda kila wakati pamoja na anuani) : ……

    ……

12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapo juu ni kweli na sahihi.

Sahihi ya Mwanafunzi: …….. Tarehe: ……

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: .....……. Tarehe: ……

FOMU YA MAELEZO YA MZAZI/MLEZI

1. Jina la Mzazi/Mlezi ……..
2. Sehemu anayoishi ……..……..…… S. L. P …….
   Namba ya Simu …….
3. Mimi Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …….

Nakiri kwamba nakubali/sikubali kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelezo mengine yatakayotolewa na Shule. Nisipotekekelza majukumu na wajibu wangu nichukuliwe hatua za kisheria na uongozi wa shule nakata. Naahisi kushirikiana na walimu na uongozi wa shule katika kuboresha taaluma ya mwanangu.

4. Tarehe …….
   Sahihi ya Mzazi/Mlezi …….
   Jina la Mzazi/Mlezi ……...

FORM (REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION) THIS FORM IS TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER

Name of pupil ……

Age …… Sex ……..

The above named has been examined is respect of:-

(a) STOOL ……..

(b) URINE …….

(c) CHEST ……..……

(d) BLOOD …….

(e) EYES ……

(f) EARS ……..……..

(g) OTHER FINDING

……

…….....

…….....

……

I am satisfied that the above named pupil is fit/not fit to pursue further studies in a Secondary school

…… **……**

SIGNATURE **DATE**

…….. **……..**

DESIGNATION **STATION**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mkoa wa …….

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya

Wilaya ……..

S. L. P ……

……..

Tarehe ……..

Mkuu wa Shule,

……..

…….

……

UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA

Nathibitisha kuwa ……. (Jina kamili la mwanafunzi) ni Raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kuandikishwa.

Baba yake (Jina Kamili) …… amezaliwa katika Mkoa wa ……. Kata ya …….

Tarafa ya ……..……. Wilaya ……

Mama yake (Jina kamili) ……. amezaliwa katika Mkoa wa …… Kata ya ……..

Tarafa ya …….. Wilaya ……. hapa nchini